# Arusha ladai makundi ...mu

mitatu huku baadhi ya wanufaika wakikosa uaminifu kiasi na kisha wanapopewa mikopo huzima simu na wengine kuhama mitaa.

"Jamani fedha hizi ni za serikali, mkizichukua rudisheni na wenzenu wengine wakope acheni tabia mbaya ya kutorejesha mikopo, oneni licha ya kuwadai Sh bilioni tatu, bado tunaendelea kutoa mikopo mengine hamjiulizi fedha hizi zinatoka wapi,"alihoji.

Kaimu Mkurugenzi Jiji la Arusha, Mwanamsiu Dossi alisema kati ya Julai hadi Desemba, Halmashauri ya Jiji la Arusha imeidhinisha utoaji wa mikopo ya Sh 565,380,410 kwa vikundi 42 vya wajasiriamali vilivyopo kata 23 jijini humo.

Alisema fedha hizo zinakopeshwa kutokana na mchango wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ambapo Sh milioni 35 zitatolewa kwa vikundi 25 vya wanawake na Sh milioni 175 zitatolewa kwa vikundi 15 vya vijana na Sh milioni 30 zinatolewa kwa vikundi viwili vya watu wenye ulemavu.

Ofisa Vijana Jiji la Arusha, Hanifa Ramadhan alisema jiji hilo litaendelea kushirikiana na vijana kuibua miradi mbalimbali na mikopo ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Aliwasisitiza vijana wanapopata mikopo kuitumia kwa uangalifu na kurejesha marejesho ili kuwezesha na wengine kukopa.

# Marekani kuleta wawekezaji mifugo, uvuvi

**Na Mwandishi Maalumu**

SERIKALI ya Marekani imeahidi kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuziinua sekta za mifugo na uvuvi ili zichangie zaidi kwenye pato la taifa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki aliyasema hayo jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada kuzungumza na Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald Wright.

Ndaki alisema Balozi Wright alimhakikishia kuwa Serikali ya Marekani ipo tayari kuleta wawekezaji kutoka nchini kwake ili kukuza na kuwezesha sekta hizo kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa viwanda.

"Balozi Wright ameahidi kuleta wataalamu kutoka Marekani ili kubadilishana uzoefu wa kiufundi katika sekta ya mifugo ili wafugaji wetu waweze kubadilika na kuanza kufuga kibiashara ili kukuza kipato chao na kuongeza ajira nchini," alisema.

Kuhusu uchumi wa bluu ambao Serikali ya Tanzania imeanza kuwekeza, Ndaki alisema Serikali ya Marekani italeta wawekezaji kuja kuwekeza katika eneo hilo na kuisaidia Tanzania kuona tija ya uwekezaji uchumi huo.

"Wenzetu wa Marekani wameendelea na wamewekeza sana katika uchumi wa bluu hivyo kupitia wao wanaweza kutusaidia kuimarisha eneo hilo ili sekta ya uvuvi iweze kuwa na tija zaidi kwa taifa letu," alisema.

Alisema pia Serikali ya Marekani ipo tayari kusaidia kukabili uvuvi haramu na alimuomba Balozi Wright aone uwezekano wa kuwapatia Watanzania nafasi ya kwenda Marekani kujifunza masuala ya mifugo na uvuvi.

Ndaki alisema Balozi Wright alikwenda kumtembelea ili kuimarisha ushirikiano katika sekta za mifugo na uvuvi, na pia kutoa salamu za pole za Marekani kwa Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kifo cha Rais John Magufuli.

Scanned with CamScanner

# Mnada wa kimataifa wa Pugu kukarabatiwa

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya kukarabati mnada wa kimataifa wa mifugo wa Pugu ili kuongeza maduhuli ya serikali.

Naibu Waziri wa Mifugo, Abdallah Ulega alisema hayo wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa (CCM) aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kukarabati mnada huo ambao ni chanzo kikubwa cha mapato ya serikali.

Ulega alisema kwa sasa serikali itakuwa inafanya ukarabati mdogo mdogo kwa kutumia fedha kidogo zilizopo wakati ikisubiri fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa mnada huo.

Akijibu swali la Mbunge Viti Maalumu, Esther Matiko (Chadema) aliyetaka kujua ni lini mnada wa mifugo wa Magena uliopo Halmashauri ya Mji wa Tarime utafunguliwa kama ambavyo serikali iliahidi mwaka 2016, Ulega alisema mnada huo ulikamilika kujengwa mwaka 1995 na ulifunguliwa mwaka 1996, ambapo ng'ombe 104,000 waliuzwa na Sh milioni 260 zilikusanywa kama maduhuli ya serikali.

"Hata hivyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mara mwaka 1997 iliagiza mnada ufungwe kutokana na changamoto zilizojitokeza ikiwamo wizi wa mifugo na sababu za kiusalama," alisema.

Alisema uongozi wa mkoa wa Mara uliwasilisha ombi rasmi wizarani la kufuta mnada wa Magena na kupendekeza uhamishiwe eneo la Kirumi Check Point.

Ulega alisema wizara hiyo ilijenga mnada wa Kirumiwa Mpakani kwa gharama ya Sh milioni 321.3 na ulifunguliwa rasmi Oktoba 16, 2018.

Alisema tangu mradi huo uanze kufanya kazi, jumla ya ng'ombe 34,855, mbuzi na kondoo 5,808 wameingia mnadani hapo na Sh milioni 428.9 zimekusanywa kama maduhuli ya serikali.

Habari Leo uk8

Tarehe 15/04/2021

Scanned with CamScanner

JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO NA MIFUGO

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA BODI YA USHAURI YA WAKALA WA ELIMU NA MAFUNZO YA UVUVI (FETA).

Kufuatia uteuzi wa **Dkt.Blandina Robert Lugendo** kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA).Waziri Wa Mifugo na Uvuvi,**Mheshimiwa , Mashimba Mashauri Ndaki,**Kwa Mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Wakala za Serikali (The executive Agencies Act) ya Mwaka 1997 Sura ya 245 ikisomwa pamoja na marejeo yake ya Mwaka 2009,Na Amri ya Rais ya Kuanzisha Wakala wa Serikali (Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi) ya Mwaka 2011,Tangazo la Serikali Na.356/2011,Amewateua wafuatao kuwa wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)

1. Profesa Zackaria Samwel Masanyiwa;
2. Dkt.Modesta Medard Ntara;
3. Bibi Prisca Jovin Ngonyani;na
4. Dkt.Robert Jeremiah Kayanda.

Uteuzi huu ni wa miaka mitatu kuanzia tarehe 29 Machi , 2021. Katibu Mkuu na Menejimenti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Sekta ya Uvuvi inawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe kwa Uteuzi huu.

**Dkt.Rashid A.Tamatamah**
**KATIBU MKUU-UVUVI**

Scanned with CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**YAH: TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA BODI YA USHAURI YA WAKALA WA ELIMU NA MAFUNZO YA UVUVI (FETA)**

Kufuatia uteuzi wa **Dkt. Blandina Robert Lugendo** kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA). Waziri wa Mifugo na Uvuvi, **Mheshimiwa, Mashimba Mashauri Ndaki,** kwa mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Wakala za Serikali (The Executive Agencies Act) ya mwaka 1997 Sura ya 245 ikisomwa pamoja na marejeo yake ya mwaka 2009, na Amri ya Rais ya Kuanzisha Wakala wa Serikali (Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi) ya mwaka 2011, Tangazo la Serikali Na. 356/2011, amewateua wafuatao kuwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA);

1. Profesa Zackaria Samwel Masanyiwa;
2. Dkt Modesta Medard Ntara;
3. Bibi Prisca Jovin Ngonyani; na,
4. Dkt. Robert Jeremiah Kayanda.

Uteuzi huu ni wa miaka mitatu kuanzia tarehe 29 Machi, 2021. Katibu Mkuu na Menejimenti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Sekta ya Uvuvi inawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe kwa Uteuzi huu.

Dkt Rashid A.Tamatamah
**KATIBU MKUU - UVUVI**

Scanned with CamScanner

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Habari Leo Uk 4

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA BODI YA USHAURI YA WAKALA WA ELIMU NA MAFUNZO YA UVUVI (FETA)

Kufuatia uteuzi wa **Dkt. Blandina Robert Lugendo** kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA). Waziri wa Mifugo na Uvuvi, **Mheshimiwa, Mashimba Mashauri Ndaki,** kwa mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Wakala za Serikali (The Executive Agencies Act) ya mwaka 1997 Sura ya 245 ikisomwa pamoja na marejeo yake ya mwaka 2009, na Amri ya Rais ya Kuanzisha Wakala wa Serikali (Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi) ya mwaka 2011,Tangazo la Serikali Na. 356/2011,amewateua wafuatao kuwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA);

1. Profesa Zackaria Samwel Masanyiwa;
2. Dkt Modesta Medard Ntara;
3. Bibi Prisca Jovin Ngonyani; na,
4. Dkt. Robert Jeremiah Kayanda.

Uteuzi huu wa miaka mitatu kuanzia tarehe 29 Machi, 2021. Katibu Mkuu na Menejimenti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Sekta ya Uvuvi inawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe kwa Uteuzi huu.

Dkt. Rashid A. Tamatamah
**KATIBU MKUU - UVUVI**

SQ000943

Scanned with CamScanner